

hatua 5

kubadili mitazamo

HATUA YA 1: KUTOJUA

Kuwa na unyonge na ulemavu ni ishara kuwa Mungu aidha hajali ama hana uwezo wa kurekebisha hali hii. Ukweli ni kwamba, huenda ikawa ni matokeo ya dhambi au utovu wa Imani. Mungu hahusiki kamwe katika maisha ya mlemavu, kwa kuwa yege hawezi kuwatumia watu ambao wamekata tamaa katika maisha. Mimi siwafahamu watu wanaoishi na ulemavu na wala sijui chochote kuhusiana na ulemavu. Mimi sina hamu ya kuwajua wala kufahamu mengi kuhusiana na maisha yao.

HATUA YA 2: HURUMA

Mimi huwahurumia sana watu walio na ulemavu. Ulemavu si jambo jema hata kidogo. kwa kweli. nimebarikiwa na Mungu na nina uwezo wa kusaidia wengine. Ninamshukuru Mungu kwa kuwa watoto wangu si walemvu. Watu walio na unyonge na ulemavu bila shaka wanahitaji mtu kama mimi kuwasaidia na kuwafanya kuwa na sababu ya kuishi kwa ajili ya shida zao. Kwa kweli sioni umuhimu wowote wala faida yoyote katika maisha yao.

HATUA YA 3: KUJALI

Kama mimi, watu walio na ulemavu waliumbwaa kwa mfano wa Mungu. Hii ndiyo sababu pekee inayowafanya wawe na dhamani. Ni matumaini yangu kuwa kuna mtu atakayewaonyesha upendo wa Mungu. Mimi nitafurahia kujungu katika juhudhi kama hizi. Kusema ukweli, tunahitaji kutafuta njia ya kuwasaidia walio na ulemavu. Labda tutahitaji kuanzisha viplndi vya kuwafunza kule kanisani pale kanisani ama hata kuwafunza wazazi wao jinsi ya kuwatunza.

HATUA YA 5: WAFANYAKAZI WENZA

Ikiwa Mungu ameita kila mmoja wetu ili tumtumikie na tumsifu kwa nafsi zetu zote, pia amafanya vivyo hivyo kwa ndugu zetu na dada zetu katika Kristo walio na ulemavu. Nadhani kuwa huduma haipaswi kuwa kwa watu walio na ulemavu bali inapaswa kufanywa pamoja na watu walio na ulemavu. Kwa pamoja tutawenza kuhimizana na kukuzana pakiwa ama pasipokuwa na ulemavu katika kila kazi njema ili tuweze kuitika wito wa Mungu. Kila mmoja wetu ana uwezo wa kupeana na pia kupokea.

HATUA YA 4: URAFIKI

Nimekuja kumfahamu na hata kutumia muda wangu na rafiki aliye na ulemavu. Hugu mtu ana dhamani machoni pa Mungu na kwangu pia. Ninajua kuwa maisha yangu yamekuwa bora kutokana na kumjua na ingawa nimekuwa wa msaada kwake, amekuwa wa baraka tele kwangu pia. Kwa kweli, sasa ningependa kuanzisha uhusiano na watu wengine wenye ulemavu. Mungu huwaleta watu mbalimbali katika kanisa langu na jamii kwa jumla wakiwemo watu walio na ulemavu na zote hunufaika tunapokuwa marafiki kwa pamoja.

KUKUZA UFAHAMU

KUTOA UFIKIAJI

KUJUMUISHA

KUHUSISHA



VISIT THE WHEATON CENTER
FOR FAITH AND DISABILITY
FOR MORE INFORMATION
AND RESOURCES.



Wheaton Center for
FAITH AND DISABILITY

"5 STAGES: CHANGING ATTITUDES" IS COPYRIGHT © 2009,
DAN VANDER PLAATS, WITH THANKS TO ELIM CHRISTIAN SERVICES,
DISABILITY CONCERN CRC AND RCA, ENGAGING DISABILITY, JONI
AND FRIENDS, AND WHEATON COLLEGE